# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA SIKONGE

SHULE YA SEKONDARI KAMAGI,
S.L.P 194,
SIKONGE

TAREHE.......................

**KUMB. NA KMSS/JIO/VOL 1/...........**

NAMBA ZA SIMU.
MKUU WA SHULE: 0735283857 /0686283857
MAKAMU MKUU WA SHULE: 0757260238/0655260238

Mwanafunzi

..........................................................................
S.L.P......................
......................................

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KAMAGI ILIYOKO KATIKA HALMASHAURI YA SIKONGE MKOA WA TABORA MWAKA 2021

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021
   Shule ya sekondari Kamagi ipo umbali wa kilomita tatu kusini mwa makao makuu ya wilaya ya Sikonge karibu na kituo cha afya Mazinge barabara iendayo Mbeya/Mpana
   Usafiri wa pikipiki /taxi/bajaji unapatikana katika kituo cha mabasi Sikonge na nauli ni pikipiki=2000/=, bajaji=2000/=
   Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 na unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia**

   **2.1.Sare ya shule**

   i. Mashati meupe mawili yenye mikono mifupi na yasiyobana mwili
   ii. Sketi mbili rangi ya kijivu kwa wasichana [**mshono ni marinda mapana**] na urefu wa sketi ni mpaka kwenye kifundo cha mguu. Kwa wavulana ni suruwali mbili rangi ya kijivu [**zisibane mwili**].
   iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na kwa wasichana visiwe na kisigino kirefu. **Haturuhusu viatu vingine vyenye urembo wa aina yoyote**
   iv. Jozi mbili za soksi **nyeupe** zisizo na mistari ya aina yoyote kwa upande wa wasichana na kwa upande wa wavulana ni soksi **nyeusi** zisizo na mistari ya aina yoyote
   v. Wanafunzi wa kiislamu; nusu kanzu nyeupe mbili za kitambaa cha tetroni nzito na hijabu [juba] nyeupe mbili ndefu zinazofunika kifua na zisizo na urembo wa aina yoyote .
   vi. Rangi ya sweta ni kijivu
   vii. Shamba dress [sketi] nyeusi mbili ndefu kwa ajili ya kushindia muda wa kazi za jioni na urefu ni kuvuka magoti. Wavulana wanatakiwa kuwa na suruwali nyeusi mbili zisizobana (chupa)
   viii. Daftari ni kaunta book **10** [quire 2] na kuendelea, Mkebe wa vifaa vya hisabati na Dictionary
   ix. Begi la madaftari 1
   x. T-shirt ya rangi ya kijivu [ataelekezwa namna ya kuipata shuleni]

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu , Sayansi na Teknolojia na Ufundi, yenye dhamana ya Elimu chini ya ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

### KANUNI NA SHERIA ZA SHULE

**Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatiamambo ya msingi yafuatayo ili kuleta ufanisi mzuri wa taasisi pamoja na matarajio mazuri yako mwenyewe**

### A. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

i. Heshima kwa uongozi ,wazazi na wafanyakazi kwa ujumla
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli zifanyikazo ndani na nje ya shule
iii. Kuwahi katika shughuli za shule utakazopewa
iv. Kufahamu na kuheshimu mipaka ya shule
v. Kutotoka nje ya shule bila sare ya shule na ruhusa ya maandishi
vi. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unaotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote. Ni marufuku kuwa bwenini wakati wa shughuli za darasani.
ix. Kuheshimu na kusimama wima bendera ya Taifa inapopandishwa na wimbo wa Taifa unapoimbwa
x. Kuishi maisha ya ushirikiano na upendo na wenzako
xi. Kutotoa matusi na lugha chafu , kuzomea au kuanzisha fujo au kushiriki katika migomo.
xii. Kusalimia wafanyakazi au mtu mtu yeyote anayestahili anapopita ndani au nje ya darasa
xiii. Kutomiliki kifaa chochote cha umeme kama vile pasi.chaja,simu .nk

xv. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

xvi. Kufanya mitihani yote ya ndani na nje.

xvii. Kuvaa kitambulisho cha shule wakati wote ndani na nje ya shule.

**3.1 .MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli na kadhalika.
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito/kupata mimba/kutoa mimba
9. Kuoa au kuolewa
10. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
11. Kufanya jaribio lolote la kujiua
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kuwa na simu ya mkononi shuleni
14. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa
15. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako,mwalimu/mlezi,na jamii kwa ujumla
16. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
17. ………………………………………………………………………………………

**4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKABIDHIWA NA MWANAFUNZI PINDI TU ANAPORIPOTI**

i. Fomu ya kupimwa afya yake [form for medical examination] ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospital ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni

ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria ,kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule

NB: Fomu zote hizi zimeambatanishwa

Tafadhali soma kwa makini maelekezo /maagizo haya na kuyatekeleza kwa kikamilifu.

Karibu sana

………………………

Yohana B. Dahaye

Mkuu wa shule

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARY KANAGI
S.L.P 194
SIKONGE-TABORA

**FORM NO. 1**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRESIDENTS' OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical Officer in respect of all Form I and Form V entrants.

Pupil's full name...........................................................................

Age/Years.........................................Sex..........................................

Blood found (red and white).......................................................

Stool examination.........................................................................

Urinalysis.......................................................................................

Venereal Diseases test..................................................................

T.B. Test:........................................................................................

Eye Test...........................................................................................

Ears..................................................................................................

Chest................................................................................................

Spleen..............................................................................................

Abdomen.......................................................................................

Urine for Pregnant........................................................................

ADDITIONAL INFORMATION (If any) eg. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc . Infection chronic or family disease etc.

.........................................................................................................................

.........................................................................................................................

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature:.......................................

**FORM NO. 2**

**SHULE YA SEKONDARI KAMAGI**

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. JINA LA MWANAFUNZI...........................................................................
2. KABILA...................................................................................................
3. TAREHE YA KUZALIWA ............MWEZI............MWAKA..............
4. AMEZALIWA KATIKA WILAYA YA ..........................................
   MKOA WA...............................................................................................
5. DINI......................................DHEHEBU.........................................
6. JINA LA MZAZI/MLEZI.............................................................................
   (Ikiwa mzazi amefariki andika jina la mlezi hapa)
7. ANWANI YA MZAZI...................................(KIJIJI)
   ..........................................(TARAFA)
   ..........................................(WILAYA)
   ........................................(MKOA)

   Na. ya simu.......................................................
8. KAZI YA BABA /MLEZI............................................................................
9. KAZI YA MAMA......................................................................................
10. Afya ya mwanafunzi (kama ana ugonjwa unaohitaji uangalizi uandikwe: taja udhaifu wowote wa mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha Daktari)
11. Majina ya ndugu wengine wanaohusika na malezi ya huyu mwanafunzi(matatu tu), anuani zao kamili na namba zao za simu
    a. Ndugu..................................................Uhusiano.............................
       ..................................................................................................
    b. Ndugu..................................................Uhusiano.............................
       ..................................................................................................
    c. Ndugu..................................................Uhusiano.............................
       ..........................................................................................

.......................................  .......................................

SAINI YA MWANAFUNZI  SAINI YA MZAZI/MLEZI

**FORM NO. 3**

**MKATABA/AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi.............................................(jina kamili) ambaye ni mwanafunzi nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii.

Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahala pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana , hivyo naahidi mbele ya wazazi /walezi wangu kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote .Naahidi kutoshiriki katika migomo , fujo, na makosa ya jinai. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.

Saini ya mwanafunzi................................................

Tarehe..........................................

Shahidi

Jina kamili................................................................................

Saini..........................................

Tarehe................................

**FORM NO. 4**

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi........ ..........................................................................(Jina kamili) ambaye ni mzazi /mlezi wa.......... ......................................................................Kidato cha .....................nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii na naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo.

Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

Saini ya Mzazi/Mlezi.................................

Anunani kamili......................................

Tarehe.............................

Simu..........................